**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

Simu:028-280-2116/4777/4778
Fax: 028-280-2330/2116
Email: das.uvinza@kigoma.go.tz
Unapojibu tafadhali taja:
**Kumb.Na.CFA.15/28/02/"F"/96**

Ofisi ya Mkuu wa Wilaya,
S. L. P. 115,
**UVINZA.**

14 Novemba, 2019

Kamisha wa Ardhi,
Wizara ya Ardhi,Nyumba na Maendeleo ya Makazi,
Barabara ya Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,
Ghorofa ya sita,
S.L.P. 2908.
**40477 DODOMA .**

**YAH: UHAWILISHAJI WA ARDHI YA KIJIJI CHA RUKOMA KUWA ARDHI YA KAWAIDA KATIKA WILAYA YA UVINZA MKOA WA KIGOMA**

Tafadhali rejea barua yenye Kumb. Na. LO/HQ/21/16 ya tarehe 16/9/2019 kuhusu kichwa cha habari hapo juu.

Kampuni ya ARMSTONE HYDRO LTD ilitambulishwa Wilayani Uvinza kwa barua yenye Kumb.Na.CCE.131/256/02/103 ya tarehe 22/1/2018 kutoka kwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Kigoma. Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Uvinza ilitambulisha kampuni hiyo katika ngazi ya Halmashauri, Tarafa, Kata na Kijiji kwa barua yenye Kumb. Na. CFA.15/28/02/C/107 ya tarehe 24/1/2018 ili kuendelea na mchakato wa kisheria.

Baada ya Halmashauri kuthibitisha kukamilika kwa mchakato wa kisheria, mnamo tarehe 10/10/2018, Kikao cha Halmashauri ya Kijiji cha Rukoma na Mkutano mkuu wa Kijiji cha Rukoma ulifanyika ili kujadili ombi la ekari 207 kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa umeme.

Wananchi waliohudhuria Mkutano Mkuu walikubali kutoa eneo la ekari 207 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa umeme. Katika Mkutano wa wananchi uliofanyika tarehe 10/10/2018 nilishiriki na kuwahoji wananchi na wakathibitisha kuwa wameridhia.

Certified true copy of the Original
Sign:......................Date:......................
BENSON KITANG'ITA KISAMARWA
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths

SIRI

Aidha katika Kikao cha Kamati ya ugawaji Ardhi ya Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza kilichofanyika tarehe 25/10/2018, wajumbe waliridhia ugawaji wa ardhi hiyo.

Hivyo nashauri ardhi ekari 207 imilikishwe kwa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na baadaye Uongozi wa ARMSTONE HYDRO LTD kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu.

Pamoja na barua hii naambatisha nakala ya Muhtasari wa tarehe 10/10/2018 wa Mkutano Mkuu wa Kijiji cha Rukoma na Halmashauri ya Kijiji na nakala ya Muhtasari wa tarehe 25/10/2018 wa Kamati ya Ugawaji ardhi, wa Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza. Pia nakala ya barua yenye Kumb.Na. UDC/D.30/28/II/55 ya tarehe 05/8/2019 kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza.

Naomba kuwasilisha.

**Mwanamyua H. Mrindoko**
Mkuu wa Wilaya
**UVINZA.**

MKUU WA WILAYA
UVINZA

**Nakala:-** Mkuu wa Mkoa,
S. L. P. 125,
**KIGOMA.**

" " Kamishna wa Ardhi Msaidizi,
Kanda ya Magharibi,
S.L.P. 342.
**TABORA.**

" " Mkurugenzi TIC
**KIGOMA.**